



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na:MTC/E.80/3VOL. I/35

27/12/2021

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA KIBARUA WA MKATABA**

**KWA KAZI YA UDEREVA**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako, anapenda kuwatangazia wataanzania wote wenye sifa tajwa hapo chini, kuomba nafasi ya kibarua wa mkataba kwa kazi ya udereva.

**DEREVA DARAJA LA II: NAFASI SABA (7) (DRIVER II)**

**SIFA ZA MWOMBAJI**

1. Awe na Cheti cha kidato cha nne(FORM IV).
2. Awe na Leseni ya Udereva Daraja la E AU C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha Ajali.
3. Awe na Cheti cha mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na VETA au chuo kingine kinachotambulika na Serikali.
4. Awe na Cheti cha majaribio ya Ufundi Daraja la II (Trade test II-Mechanics).

**KAZI NA MAJUKUMU**

1. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
2. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.
3. Kufanya usafi wa gari.
4. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
5. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
6. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali, na
7. Kufanya kazi nyingine kadri utakavyoelekezwa na msimamizi wake.

**NGAZI YA MSHAHARA**

TGS B<sub>1</sub>, TSHS. 390,000/= Kwa Mwezi.

**MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE AMBAYO NI YA LAZIMA  
KUZINGATIWA**


1. Mwombaji ni lazima awe ni Raia wa Tanzania.
2. Awe hajawahi kufungwa kwa makosa ya jinai.
3. Maombi ni lazima yaambatanishwe na vivuli vya vyeti vya kuzaliwa, kuhitimu Elimu ya Sekondari na vyo vya mafunzo/tauluma vinavyotambuliwa na Serkali.
4. Awe na Umri usiozidi miaka 45.
5. Maombi lazima yaambatanishwe na picha 2 za Passport size za hivi karibuni
6. Maombi lazima yaambatanishwe na CV (Curriculum Vitae) (Wasifu).
7. Awe na umri wa zaidi ya miaka 18.
8. Hati za matokeo za kidato cha nne na hati za vyeti vya taaluma havitapokelewa.
9. Watakaoitwa kwenye usaili watajigharamia wenyewe.
10. Maombi yanaweza kuandikwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili au Kiingereza.
11. Awe tayari kufanya kazi eneo lolote atakalopangiwa ndani ya Halmashauri ya Mji Makambako.
12. Awe na wadhamini wawili (2) ambao ni watumishi wa Serikali.
13. Barua za wadhamini zipitishwe kwa waajiri wao.

**MAOMBI YOTE YATUMWE KWA ANUANI IFUATAYO:-**

MKURUGENZI,  
HALMASHAURI YA MJI,  
S.L.P 405,  
MAKAMBAKO.

**MWISHO WA KUTUMA MAOMBI NI TAREHE 10/01/2022**

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:-**



Kenneth K. Haule

**MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI**

MKURUGENZI  
HALMASHAURI YA MJI  
MAKAMBAKO

---

Halmashauri ya Mji Makambako, Mtaa wa Sigrud, Barabara kuu ya Njombe, S.L.P 405  
Makambako, Njombe, Nukushi Na: 026-2968891, Simu Na: 026-2968892,  
Barua Pepe: [td@makambakotc.go.tz](mailto:td@makambakotc.go.tz), Tovuti: [www.makambakotc.go.tz](http://www.makambakotc.go.tz)